AJIRA ZA WATAALAM WA KITANZANIA KWENYE MASHIRIKA YA KIMATAIFA

1.0 UTANGULIZI:

Wataalam wa Kitanzania kuajiriwa katika Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Jumuiya nyingine za Kimataifa ambazo Tanzania ni mwanachama, ni jambo linalokubaliwa na kuungwa mkono na serikali.

1.2 Mbali ya kuwa ni moja ya maeneo ya kuwapatia kazi wananchi wetu, ajira katika mashirika hayo pia zinatoa nafasi ya kuongeza upeo, ujuzi na uzoefu na hivyo kuwaendeleza wataalam hao kwa manufaa yao wenyewe, mashirika yao na vile vile kulijengea uwezo Taifa.

1.3 Wataalam wa Kitanzania wanaoajiriwa na Mashirika ya Kimataifa wanatazamiwa kuwa wawakilishi wa Taifa katika mashirika hayo. Aidha kuwepo kwao kwenye mashirika hayo, kutachangia katika utambuzi wa maslahi ya nchi na vipaumbele vya maendeleo vya Taifa letu vinavyoweza kuchangiwa na mashirika hayo.

1.4 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ndiyo yenye dhamana ya kuratibu na hivyo uhamasishaji wa ajira za wataalam wazalendo kwenye mashirika ya kimataifa kwa kuzitangaza nafasi wazi katika mashirika haya mara zinapotokea.

2.0 MAMBO YA KUZINGATIWA:

2.1 Wataalam wa Kitanzania walioko katika utumishi wa umma ambao wataomba na kufanikiwa kupata kazi kwenye mashirika ya kimataifa, wanaruhusiwa kuomba likizo bila malipo kwa kipindi watakachokuwepo huko.

2.2 Utaratibu wa Likizo bila malipo na kushikizwa umeainishwa katika nyaraka mbalimbali za serikali ambazo ni pamoja na Waraka wa watumishi wa serikali na 5 wa mwaka 1986,

waraka wa utumishi namba 9 wa mwaka 1992, Kanuni H.25(a) na Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma Toleo la mwaka 1994 na Kanuni 99 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na waraka Kumb. Na.C/AC/44/45/01/A/47 wa Aprili 4, 2006.

2.3 Kwa mujibu wa nyaraka hizo, Katibu Mkuu, Ofisi ya rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiye mamlaka ya kuidhinisha maombi ya vibali vyote vya Likizo bila malipo na kushikizwa yanayowasilishwa moja kwa moja na mwajiri au mtumishi mwenyewe kupitia kwa mwajiri wake kwa idhini.

2.4 Maombi hayo yatashughulikiwa kwa Utaratibu ufuatao:-

2.4.1 Sharti yaidhinishwe na mwajiri mwenyewe au afisa anayekaimu nafasi yake.

2.4.2 Yawasilishwe Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na viambatanisho muhimu kama vile mkataba wa kazi, maelezo yenye kuonyesha faida itakayopatikana kwa umma iwapo mtumishi huyo ataruhusiwa kuchukua Likizo hiyo.

2.4.3 Yafafanue bayana kazi za mtumishi anayetaka kuchukua Likizo bila malipo zitafanywa na nani.

2.4.4 Yafafanue endapo nafasi iliyoachwa wazi ni muhimu kuendelea kuwepo au ifutwe kutoka ikama ya taasisi.

2.5 Endapo maombi ya Likizo bila malipo yatakubaliwa, kipindi cha juu cha mtumishi ni miaka mitatu. Muda huo unaweza kuongezwa kwa watumishi watakaoiwakilisha nchi katika mashirika ya Umoja wa mataifa/Umoja wa Afrika/nchi za SADC/taasisi za Jumuiya ya Madola au nyinginezo ambazo Tanzania ni mwanachama. Aidha, urejeaji kazini baada ya kumalizika kwa vibali hivyo utategemea kuwepo kwa nafasi wazi za kuwapokea.

2.6 Iwapo nafasi aliyoiacha itakuwa imejazwa, mtumishi huyo atalazimika kuomba kazi upya serikalini. Hivyo ajira itategemea kuwepo kwa ikama yenye fedha.

2.7 Baada ya kuzingatia Utaratibu huu, wataalam wa Kitanzania mnahamasishwa kuomba nafasi katika mashirika ya Kimataifa mara zitakapotangazwa. Aidha mnatakiwa kupitia tovuti za mashirika hayo mara kwa mara ili kuona nafasi zinazotangazwa na kuziomba. Watanzania watakaoomba nafasi hizo moja kwa moja kupitia tovuti za mashirika hayo – wanashauriwa kutuma Nakala ya maombi hayo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

2.8 Umuhimu wa kupitisha maombi au kutuma nakala ya maombi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kuweza kupata idhini ya serikali pale ambapo idhini hiyo ni kigezo katika kumfikiria muombaji kwa kazi anaoyoiomba kutokana na makubaliano baina ya serikali ya Jamhuri ya Muungano na shirika au jumuiya ya kimataifa.

2.9 Aidha waajiri wanasisitizwa kuwahamasisha watanzania kwa kuwatambua watumishi wenye sifa, kuomba kazi zinazolingana na uwezo wao katika mashirika haya na kuwaruhusu kuchukua likizo bila malipo kwa mujibu wa kanuni na taratibu.

2.10 Anuani na tovuti za baadhi ya Mashirika ya Kimataifa yanayotoa nafasi hizo mara kwa mara, zinapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma : www.estabs.go.tz .

ANUANI NA TOVUTI ZA MASHIRIKA YA KIMATAIFA YANAYOTOA NAFASI ZA KAZI

S/N	INSTITUTION NAME	ADDRESS/E-MAIL	PHONE NO/FAX
1.	Southern African Development Community Secretarial (SADC)	Private Bag 0095 Gaborone Botswana E-mail: registry@sadc.int Website: www.sadc.int	**Phone**: (267) 3951863 **Telefax**: (267) 3972848 (267) 3181070
2.	United Nations (UN)	201 East 42 NO. Street, Suite 1700 New York, New York 10017 E-mail: tzrepny@aol.com	**Tel**: (212) 972-9160 **Fax**: (212) 682-5232 **Website**: http.jobs.un.org
3.	United Nation, Scientific and Cultural Organization (UNESCO)	Secretary General UNESCO National Commission P.O. Box 20384 **DAR ES SALAAM** 13 AV.Raymond Poincare 75116 Paris France E-mail: embtanzanie@wanadoo. fr:dl.tanzanie@unesco.org Website:www.amb_tanzanie.fr www.unesco.org/employment	**Telephone**: 0153706366 **Fax**: 0147550546
4.	World Intellectual property Organization (WIPO)	WIPO 34 chemin des doubetes 1211 Geneva 20, Switzerland, E-mail: staffengagements @wipo.int Website: www.wipo.int	**Tel**: (41.22) 338.91.11 **Fax**: (41.22) 338.98.20
5.	Indian Ocean Rim Association for Regional Cooperation (IOR-ARC) Secretarial	Deputy Foreign Minister for economic affairs Ministry of foreign affairs Islamic Republic of Iran Kooshk Mesri street Tehran Iran E-mail: Mecd@mfa.gov.ir	Fax: +98-21-61153356
6.	United Nations Environment Programme (UNEP)	Executive Office P. O. Box 30552 **Nairobi – Kenya** Re-insurance plaza (9th floor Taifa Road) P.O. Box 47790 GPO 00100 **Nairobi Kenya** E-mail: executiveoffice@unep.org :highcom@tanzamahc.or.ke Website: www.unep.org/vacancies	Phone: 312027-311948, 311950 Telegrams: TANZAREP NAIROBI Fax: 218269 (25420) 7624275/4008

S/N	INSTITUTION NAME	ADDRESS/E-MAIL	PHONE NO/FAX
7.	Food and Agriculture Organization of the United Nations (FAO)	Chief, AFDs FAO viale delle terme di caracalla 00100 **Rome Italy** E-mail:AFDs Registry@fao.org RNE-VA-1648@fao.org	Fax.No.+390657055022 +390657055749
8.	African Union (AU)	Addis Ababa Ethiopia P. O. Box 3243 E-mail recruits@africa-uion.org Website: www.africa-union.org	Telephone: (251-11) 5517700 Fax No: (251-11) 5510430 00251-1-525840/510430
9.	Commonwealth Secretariat	Marlborough house pall London SWTY 5 HX Website: www.thecommonwealth.org	Fax: +44(0)2079300827
10.	International Criminal Court (ICC)	E-mail: applications@icc-cpi.int Website: www.icc.cpi.int/jobs/vacancies/750.html	
11.	The East African Community (EAC)	Secretary General EAC AICC Building P. O. Box 1096 ARUSHA	**Tel**: +255-27-2504253-8 **Fax**: +255-27-2504255/2504481
12.	The World Bank	1818 H Street, NW Washington DC 20433 USA	**Tel**: (202) 473-1000 **Fax**: (202) 477-6391